(١)

Ramadhani ni mwezi wa kufanya wema, kuunganisha undugu na kupata rehma za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Prof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa viumbe vyote. Anaesema katika Kitabu chake Kitukufu:

{لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ}

{Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake.

Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote. Na mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu:

Hakika ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani uliobarikiwa, huu ni Mwezi wa Utiifu, Tunu na Rehma nyingi. Na ni Mwezi wa kufunga na kuswali Usiku, Kuunganisha undugu na Upendo, na Kushirikiana katika Mema na Uchamungu. Ni mwezi ambao ndani yake Mja hupimwa Uvumilivu wake, na jinsi anavyomtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu na anavyomwogopa. Mwenye Swaumu huvumilia Njaa na Kiu, na huyazua matamanio ya nafsi yake, na huvumilia kila aina ya Maudhi, pamoja na kujikurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kila aina ya utiifu; kama vike kuisoma Qurani Tukufu, kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuswali Usiku, kutoa Sadaka, kuwasuluhisha Watu, na kujitahidi katika kila jambo la heri ambalo lina masilahi kwa Nchi na watu, na hivyo ni kwa kufanya Wema unaomletea mja huruma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِنَ الْمُحْسِنِينَ}

mema fanya wanao na karibu iko Mungu Mwenyzi ya rehema Hakika

Na anasema Mtume S.A.W: Hakika ya heri hii ina hazina nyingi, na katika hazina hizo kuna funguo nyingi, na kwa hiyo uzuri ulioje kwa mja aliyejaaliwa ufunguo wa heri na Mwenyezi Mungu Mtukufu, ukawa ndio kifungio cha Shari. Na ole wake mja ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu amemjaalia ufunguo wa Shari, ukawa ndio kifungio cha Heri.

Hakika ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani uliobarikiwa ni uwanja wa kushindana kwa vitendo vya heri na wema, ambapo Waja hushindana ndani ya mwezi huu kwa matendo yenye nia njema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ilikuwa ndio hali yake Mtume S.A.W ndani ya Mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kutoka kwa Ibnu Abas R.A amesema: Mtume S.A.W alikuwa Mbora wa kutoa katika Watu, na Ubora wake wa kutoa ulikuwa zaidi ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani pindi anapokutana na Jiburilu. Na alikuwa anakutana naye kila siku katika nyusiku za mwezi mtukufu wa Ramadhani, na akawa anamfundisha Quran Tukufu. Kwa hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, S.A.W alikuwa Mtoaji mzuri wa mambo mazuri kuliko kasi ya kimbunga. Kwa hiyo, Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni Uwanja mpana wa kufanya Mema, na hasa kulisha chakula ambacho ni katika alama nzuri za Mwezi huu Mkarimu, na ni alama miongoni mwa alama za Dini yetu tukufu. Anasema Bwana wetu Abdallah bin Salaam, R.A: Mtume Muhammad S.A.W alipokuja Madina, watu walimzunguka na Mimi nikawa miongoni mwa hao waliomzunguka, na nilipouona uso wake, nikajua kuwa huo sio Uso wa mwongo. Kisha nikamsikia akisema: Enyi Watu, lisheni chakula, na toeni Salamu, na unganisheni undugu, na mswali wakati Watu wamelala, mtaingia Peponi kwa amani. Maneno ya Mtume S.A.W yameyakusanya mambo manne. Matatu kati ya hayo yanahusiana na mtangamano na Watu, nayo ni: Kulisha chakula, kutoa salamu, na kuunganisha undugu. Na jambo la nne linahusu uhusiano wa Mja na Mola wake, nalo ni: kuswali Usiku wakati watu wamelala. Na Mtu mmoja alimuuliza Mtume S.A.W: Ni upi Uislamu ulio bora zaidi? Akasema S.A.W: Lisha chakula, toa salamu kwa umjuaye na usiyemjua. Na Mtu hapaswi kudogesha au kudharau kitu chochote katika wema, kwani yeye hajui ni amali ipi inayokubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Anasema Mtume wetu S.A.W: Usidharau chochote katika Wema, hata kama utatoa kiunganishi cha kamba, au ukatoa hata kijikamba

cha kiatu, au hata ukayapunguzia maji yako kwenye chombo cha mteka maji,

‘

Hata kama kwa Kuondosha kitu njiani ili kisiwaudhi watu, au ukakutana na ndugu yako hali ya kuwa uso wako kwake mkunjufu, na kama utakutana na ndugu yako ukamsalimia, au ukamliwaza mpweke duniani, na iwapo mtu atakutukana kwa kitu chochote anachokijua kuhusu wewe, na wewe unamjua yeye fika, basi usimtusi ili ujipatie malipo yake na yeye abebe mzigo wa dhambi, na kile ambacho masikio yako yatapenda kukisikia basi ukifanye, na kile kitakachochukiwa kusikiwa na masikio yako basi ujiepushe nacho. Na anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu S.A.W: Kila muislamu anapaswa atoe sadaka. Akasema: umaonaje kama hatakuwa na cha kutoa? Akasema: afanye kwa mikono yake, ajinufaishe na atoe sadaka. Akasema: Na kama hakuweza kufanya hivyo? Akasema: amsaidie mwenye shida nzito. Akasema: Unaonaje iwapo atashindwa kufanya hivyo? Aamrishe heri au Uadilifu. Akasema: Unaonaje iwapo atashindwa kufanya hivyo? Akasema: ajizuie na Shari ya aina yoyote; kwa kufanya hivyo atakuwa ametoa sadaka.

Hakika sisi tunatilia mkazo kwamba wema ni jina linalokusanya kila Jambo zuri na kila kitendo kinachomridhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwanufaisha watu. Na yote hayo yanakusanyika katika Tabia njema. Na kwa ajili hiyo, amesema Mtume S.A.W: Wema ni Tabia njema. Kama ambavyo, Uaminifu na Kutambua fadhila na Jema kwa waliokufanyia ni katika Maadili halisi hawajipambi nayo isipokuwa Watu wenye maadili.

Miongoni mwa sura bora za wema ni kuunganisha undugu na Mawasiliano baina ya Watu wa nyumbani, ndugu wa karibu na wa mbali, Majirani na Watu wote na jambo hili ni katika visaidizi vikubwa mno vya kuleta Mjongeleano, kuhurumiana na kufungamana, lakini

pia kueneza Maadili ya kuhurumiana baina ya watu wote. Na mwezi mtukufu wa Ramadhani ni mwezi usiokuwa na nafasi ya wenye kuleta migongano na migongano yenyewe. Na kwa kuwa mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa kuunganisha undugu, basi katika kuunganisha undugu huo kuna mambo mawili muhimu: Kuunganisha undugu wa karibu. Na Mtume S.A.W amebainisha kiwango na nafasi ya undugu huo katika Hadithi Qudsiy anayoisimulia kutoka kwa Mola wake: anapokaa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu: Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, na Mimi ni Mwingi wa kurehemu. Nimeuumba Undugu (wa kuzaliwa pamoja) na nikaupa sehemu ya Jina langu. Na yoyote atakayeuunganisha na mimi nitamuunganisha, na yoyote atakayeukata na mimi nitamkata. Kisha Mtume wetu S.A.W akasema:

Na mnapopoteza matumaini basi isomeni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

{فهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ * أُولَئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعْمَى أَبْصَارَهُمْ * أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَى قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا}

{Basi yanayo tarajiwa kwenu mkitawala ndio mfisidi katika nchi na mwatupe jamaa zenu? Hao ndio Mwenyezi Mungu alio walaani, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao. Je! Hawaizingatii hii Qur'ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?}

Na anasema Mtume wetu S.A.W: Matendo ya Waja huwekwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kila siku ya Jumatatu na alhamisi, na Mwenyezi Mungu Mtukufu humsamehe ndani ya siku hizi mbili kila

mtu asiyemshirikisha yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu na kitu chochote isipokuwa alikuwa na jambo la ugomvi baina yake na nduguye, ataambiwa: waacheni wawili hawa mpaka wapatane.
Na Mtume S.A.W amekujaalia kuunganisha undugu kuwa ni katika misingi muhimu ya Imani aliyoilingania Mtume S.A.W mwanzoni mwa kupewa kwake Utume. Na kutoka kwa Amru bin Absah amesema: Niliingia nyumbani kwa Mtume S.A.W, yaani mwanzoni mwa Utume wake, nikasema: Ni nani wewe? Akasema: Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nikasema: Ni nini maana ya Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu? Akasema: Ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Je? Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyekutuma? Akasema: Ndio. Akasema: ili apwekeshwe Mwenyezi Mungu Mtukufu, na asishirikishwe na kitu chochote, na kuvunja vunja Masanamu, na kuunganisha undugu. Na Mtume S.A.W amejaalia kuunganisha undugu kama ni alama miongoni mwa alama za Imani. Akasema: Na anayemwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Siku ya Mwisho basi na aunganishe undugu wake.

Na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inathibitisha hivyo, anaposema:

{وَأُوْلُواْ الأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَى بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ الله}.

{Na jamaa wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe zaidi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu}.

Upande mwingine wa kuunganisha, ni kuwaunganisha Watu wote wanaokuzunguka. Usimkate mtu yoyote. Mtume S.A.W anasema: Haiwi halali kwa mtu kumuhama ndugu yake zaidi ya Siku tatu. Wanakutana na na kila mmoja anamkwepa mwenzake, na Mbora wao ni yule atakaye anza kwa salamu.
Haimaanishi aanze kwa salamu tu anapokutana na ndugu yake, bali kwa maana ya kuanza kwa maamkizi ya kweli yaliyomo katika salamu

hiyo kwa ujumla wake. Iwe salamu hiyo, ni ya kweli sio ya juu juu juu, inayotoka katika ulimi ikikanushwa na moyo, bali iwe salama inayotoka moyoni, unapokuwa na Rafiki, Watu wako wa nyumbani, Jirani, mtumishi mwenzako, au mwanadamu yoyote, au wanyama, vitu mbalimbali, pamoja na ulimwengu kwa ujumla.

Ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَافَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِين}.

{Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu, wala msifuate nyayo za She'tani; hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi}.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

* * *

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na ninashuhudia kwamba hakuna yoyote anayestahili kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye pekee asiye na mshirika wake, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu Muhammad ni Mua na ni Mtume wake, na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu.

Hekima ya Mwenyezi Mungu Mtukufu imepelekea kuzifanya siku kumi za mwisho za Mwezi wa Ramadhani kuwa ni fursa kubwa kwa mja mwema kuongeza mema yake na mja mwenye upungufu wa Mema aweze kuyadiriki mema yaliyompita . Hizi ni siku zenye tunu nyingi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na Upaji wake kwa wingi ambao yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu amewatunuku waja Wake. Ikawa ni bora kwa kila Muislamu kukutana na Rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya siku hizi za Mwisho za Mwezi wa Ramadhani. Anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika Mola wenu katika siku za Mwaka wenu, ana tunu, basi zijongeleeni tunu hizo: huwenda mmoja wenu akaipata tunu moja, ikamfanya asiasi tena milele baada yake.; Kwa hiyo, Mtume S.A.W alizitenga siku kumi za mwisho wa Ramadhani kwa kuongeza Ibada, Utiifu, na kumwelekea Mola wake Mtukufu kwa wingi.

Na katika mambo tunayotakiwa kuyapupia ni kuuhuisha Usiku kwa kumfuata Mtume S.A.W. Mtume S.A.W alikuwa anajitahidi sana katika siku hizi kumi kuliko alivyokuwa alijitahidi katika siku zingine. Kutoka kwa Mama wa Waumini, Bi Aisha R.A, anasema: Mtume S.A.W alikuwa, pindi linapoingia kumi la mwisho la mwezi Mtukufu wa Ramadhani, alikuwa akizitilia akiwaepuka wakeze, na akihuisha usiku wake na kuwaamsha watu wake wa nyumbani. Na kutoka kwa Bi Aisha pua katika mapokezi mengine. Mtume S.A.W alikuwa akichanganya katika siku ishirini za mwanzo, kulala na kufanya Ibada, na linapoingia kumi la mwisho alizidisha bidii kwa kufanya ibada nyingi zaidi

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amezitengea siku kumi za mwisho wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, usiku Mbora wa nyusiku zote kwa fadhila zake nyingi. Nao ni Usiku wa Cheo, amefanya hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya utukuzaji kutoka kwake kwenda kwa Umma wa Kipenzi chake S.A.W. Kutoka kwa Mujahid R.A: Kwamba

Mtume S.A.W alimtaja Mtu Mtu mmoja wa Kizazi cha Waisraeli aliyebeba silaha kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu miezi elfu moja, akasema: Waislamu wakashangazwa na jambo hilo, akasema:

Basi, Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha sura hii:

{إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ * وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ * لَيْلَةُ الْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ * تَنَزَّلُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِنْ كُلِّ أَمْرٍ * سلام هِيَ حَتَّى مَطْلَعِ الْفَجْرِ }

{Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'ani katika Laylatul Qadri, Usiku wa Cheo Kitukufu. Na nini kitacho kujuulisha nini Laylatul Qadri?Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na Roho katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi kwa kila jambo. Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri}.
Kwa hiyo, Ibada ndani ya Usiku huu kwa nia safi, inaizidi Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, tena kwa muda wa miezi elfu moja katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Na Mtume S.A.W amesema kwamba Kuswali ndani ya Usiku huu ni sababu ya kusamehewa madhambi yote. Anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakayeswali Usiku wa Cheo kwa Imani na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, atasamehewa madhambi yake yote aliyoyafanya. Na kwa ajili hiyo, Muislamu anapaswa kupupia katika kuuhuisha usiku huu uliotukuzwa, kwa ajili ya kujikurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, akiwa na matumaini ya kusamehewa madhambi yake yote. Na Mtume wetu S.A.W ametuasa tuutafute Usiku huu wa Cheo katika masiku ya Witri ya kumi la mwisho la mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na kuwepo ndani yake wiki wa Upaji wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja wake pamoja na ukarimu wake kwao. Anasema Mtume S.A.W:

Utafuteni Usiku wa Cheo katika Masiku ya Witri ya kumi la mwisho la mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Na katika mapokezi mengine, anasema Mtume S.A.W: Utafuteni Usiku wenye Cheo, katika siku kumi za mwisho za Mwezi mtukufu wa Ramadhani, inakuwapo katika siku ya tisa, au katika siku ya saba, au katika siku ya tano. Kwa maana ya kuitafuta ndani ya siku za Witri.

Na miongoni mwa kazi nzuri na bora katika siku hizi ni utoaji wa zaka ya Fitri ambayo ni usafishaji wa mfungaji na ni kilisho cha mafukara na masikini. Kutoka kwa Ibnu Abas R.A amesema: Mtume S.A.W alifaradhisha Zaka ta Fitri kwa lengo la kumsafisha mfungaji kutokana na mambo ya kipuuzi na maneno mabaya. Na ni kwa ajili ya kuwalisha mafukara na masikini. Na atakaeitekeleza kabla ya Swala ya Eid, basi hiyo itakuwa imekubaliwa. Na atakaeitekeleza baada ya swala ya Eid, basi hiyo itakuwa ni sadaka miongoni mwa Sadaka.

Na miongoni mwa Matendo bora ni: kujitahidi kwa Dua. Kwa kuwa Dua ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani ina matumaini makubwa ya kukubaliwa, basi katika kumi la mwisho lina nafasi kubwa zaidi ya Dua Kukubaliwa. Na kutoka kwa Mama wa Waumini, Aisha R.A amesema: Nilimwambia Mtume S.A.W, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: Unaonaje iwapo mimi nitaugundua usiku wenye cheo, ni nini cha kukisema ndani ya usiku huo? Akasema Mtume S.A.W: sema: Ewe Mola wangu, hakika yako Wewe ni Mkarimu na Msamehevu unapenda kusamehe, basi ninakuomba unisamehe. Basi tupupie katika kuzitumia siku hizi zenye fadhila nyingi pamoja na Usiku wenye cheo uliobarikiwa, kwa kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa kuomba Dua na Kusoma Qurani Tukufu kwa wingi, lakini pia kwa kufanya kila kinachotukurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, mpaka pasiwepo Mtu yoyote mwenye kunyimwa Rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya usiku huu, kwani hakika kunyimwa Rehema ndani ya Usiku huu ni kunyimwa kweli kweli. Anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika Mwenyezi Mungu

Mtukufu ndani yake ana Usiku ulio bora kuliko Miezi elfu moja, atakayenyimwa Kheri zake atakuwa amenyikwa kweli kweli.

.

Ewe Mola wetu hakika Wewe ni Msamehevu unaependa kusamehe, tunakuba utusamehe.